SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

MUHUTASARI WA ELIMU YA MSINGI

SOMO LA SANAA ZA UBUNIFU NA MICHEZO

DARASA LA I – III

2022

© TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2022

Toleo la Kwanza 2022

Umesanifiwa na kuandaliwa na;

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ)

S.L.P 840,

Mazizini,

Zanzibar.

Barua Pepe: info@zie.go.tz

Tovuti: www.zie.go.tz

Simu: +255-24-2230193

ISBN: 978-9912-754-21-8

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kurudufu nyaraka hii kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

YALIYOMO

DIBAJI..... iv

SHUKURANI.....**v**

1.0 UTANGULIZI.....vi

1.1 Falsafa ya Elimu Zanzibar.....vi

1.2 Madhumuni ya Elimu Zanzibar.....vi

1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi vii

1.4 Sababu za Kupitia Mtaala wa Msingi vii

1.5 Umuhimu wa Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo..... viii

1.6 Matokeo ya Jumla ya Kujifunza Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo. viii

2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI..... viii

2.1 Kurasa za Awali viii

2.2 Jaduweli la Ujifunzaji ix

2.2.1 Mada ix

2.2.2 Matokeo Mahususi ya kujifunza ix

2.2.3 Mbinu za Kujifunzia ix

2.2.4 Nyenzo za kujifunzia ix

2.2.5 Upimaji ix

2.2.6 Vipindi x

2.3 Mawanda na Mtiririko x

DARASA LA KWANZA 1

DARASA LA PILI 15

DARASA LA TATU 30

DIBAJI

Muhutasari wa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo wa darasa la I-III wa mwaka 2022, unatokana na mabadiliko makubwa ya kielimu yaliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) ambayo yamehusisha kazi ya upitiaji wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi ulioandikwa mwaka 2019. Madhumuni ya kupitia mtaala huo ni kuufanya uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira pamoja na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni kama inavyoelezwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar.

Kutokana na mabadiliko ya mfumo wa elimu Zanzibar, yaliyopelekea kurejeshwa kwa darasa la saba ikiwa ni miongoni mwa uimarishaji wa elimu ya Msingi, kwa sasa elimu ya Msingi itakuwa ni miaka 7 badala ya miaka 6 ya awali. Kwa kuzingatia mabadiliko hayo, WEMA kupitia Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ) imeandika muhutasari wa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo ili kukidhi mahitaji ya taaluma hiyo. Kwa hivyo, muhutasari huu umekusanya mada za somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo ambazo zinaendana na maudhui na muktadha wa somo hili.

Kazi ya uandishi wa muhutasari huu imejumuisha wadau mbalimbali wa elimu katika ngazi tafauti hususan elimu ya Msingi. WEMA kupitia TEZ imehakikisha kuwa muhutasari umezingatia vyema maoni ya wadau hao, pamoja na mapitio ya machapisho mbalimbali kutoka nchi nyengine zinazofanana kijiografia, idadi ya wakaazi na mifumo ya elimu.

WEMA inatoa shukurani za dhati kwa wadau wote waliochangia katika kuandaa muhutasari huu wa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo wa darasa la I-III wakiwemo; Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi, Uongozi na Watendaji wote wa TEZ, Jopo la Wataalamu, Wakuza Mitaala, Walimu na wastaafu mbalimbali wa WEMA walioshiriki katika matayarisho ya muhutasari huu hadi kukamilika kwake. Ni matumaini ya WEMA kuwa, muhutasari huu utatumika kwa skuli zote za Zanzibar za Serikali na binafsi pamoja na watekelezaji wengine katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

Khamis A. Said.
Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Zanzibar.

SHUKURANI

Taasisi ya ELimu ya Zanzibar (TEZ) inatoa shukurani za dhati kwa Mh. Leila Muhamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mh. Ali Abdulghulam Hussein, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Nd. Khamis Abdulla Said, Katibu Mkuu WEMA, Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na Dkt. Abdullah Ismail Kanduru; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TEZ.

Shukurani za pekee ziwaendee wakuu wa divisheni wa TEZ, wafanyakazi wote wa TEZ na Wajumbe wa Bodi ambao walikuwa ni washiriki wa kazi ya utayarishaji wa Muhutasari huu. Pia, shukurani ziwaendee maafisa wa ngazi tafauti katika Wizara ya Elimu kwa kutumia muda wao na kutoa maoni kuhusu mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika uandaaji wa Muhutasari huu. Kwa kuongezea TEZ inawashukuru walimu wote, wazazi na wanafunzi kwa kushiriki katika kazi hii.

Pia, TEZ inazishukuru taasisi mbalimbali kwa kuruhusu watendaji wao kufanya kazi na TEZ. Taasisi zenyewe ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Abdurahman Al -Sumait, Madrasa Early Childhood Programme Zanzibar (MECP-Z) na Mamlaka ya Mji Mkongwe, Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Tume ya Dawa za Kulevya, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Hospitali ya Mnazi Mmoja na Ofisi ya Mufti Mkuu. Taasisi nyengine ni Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Chuo cha Kiislamu, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, Idara ya Elimu ya Sekondari, Jumuia ya Skuli Binafsi na Taasisi nyengine zilizoshiriki katika kufanikisha upatikanaji wa Muhutasari wa Elimu ya Msingi.

Mwisho, TEZ inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo hususan GPE kwa kutoa mchango wao wa hali na mali katika kukamilisha kazi hii.

Abdalla M. Mussa.
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar,
Zanzibar.

UTANGULIZI

Muhutasari wa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo umeandaliwa kwa wanafunzi wa darasa la I-III ambao umechukuwa nafasi ya muhutasari wa somo la Michezo kwa ngazi ya Msingi Darasa la I-VI na Elimu Amali la darasa la V-VI wa mwaka 2009. Muhutasari huu umejumuisha sehemu ya Utangulizi, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo na Madhumuni ya Elimu ya Zanzibar, Sababu za kupitiwa mtaala na umuhimu wa kujifunza somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo. Pia, muhutasari huu umejumuisha Matokeo ya Jumla ya Kujifunza somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo, Muundo wa Muhutasari, Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa kila darasa pamoja na Jaduweli la Muhutasari.

1.1 Falsafa ya Elimu Zanzibar

Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi unakwenda sambamba na falsafa ya elimu ya Zanzibar, kwa kuzingatia mila na misingi ya mfumo wa elimu hiyo.

Falsafa ya elimu ya Zanzibar ni sawa na ile ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inalenga katika falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea. Falsafa hii, inajumuisha kujitegemea, kujiamini, uendelevu, kuwa na stadi za maisha, kuthamini usawa, ujasiriamali, uvumbuzi, udadisi, ubunifu na uwezo wa kutathmini na kuchambua.

1.2 Madhumuni ya Elimu Zanzibar

Yafuatayo ndiyo madhumuni ya elimu Zanzibar:

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, ujuzi na mwelekeo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.
5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi

Yafuatayo ndiyo madhumuni na malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar:

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.
2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.
3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi, fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu na mataifa mengine.
11. Kuwezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na kufahamu hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.
12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi kwa mazingira wanamoishi pamoja na utashi.

1.4 Sababu za Kupitia Mtaala wa Msingi

Mnamo mwaka 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi. Madhumuni yalikuwa ni kuufanya mtaala uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira pamoja na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni, kama inavyoelezwa katika nyaraka

mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar, inayolenga kuimarisha ubora na muundo wa elimu ili kuwa na muunganiko mzuri unaoanzia Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kwa kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Miongoni mwa mabadiliko yaliyopendekezwa ni kuwa na miaka saba (7) ya elimu ya msingi badala ya miaka sita (6) ya awali.

1.5 Umuhimu wa Kujifunza Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo

Katika mapitio yaliyofanywa mwaka 2019 ilibainika kwamba somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo halikuwepo bali maudhui yake yalikuwa kama mada katika masomo ya Elimu Amali na Michezo. Kutokana na mahitaji ya jamii, imeonekana ni vyema somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo liweze kujitegemea kuanzia darasa la I - VII. Hii ni kwa sababu, somo hili humsaidia mwanafunzi kumjengea maarifa, stadi na mwelekeo chanya wa kumuwezesha kucheza na kubuni shughuli zitakazomwezesha kujitegemea. Pia, somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo linamsaidia mwanafunzi kuimarisha afya yake kwa kutekeleza stadi za ujasiriamali, kuweza kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza. Zaidi, somo hili linamsaidia mwanafunzi katika kuendeleza mila na desturi za Kizanzibari.

1.6 Matokeo ya Jumla ya Kujifunza Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo

Baada ya kusoma somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo katika skuli za msingi, mwanafunzi ataonesha ujuzi wa:-

1. Kuthamini na kufanya kazi za amali zenye tija.
2. Kuthamini kazi za ubunifu za kijamii na kujielezea kiubunifu kupitia matendo mbalimbali ya kisanaa.
3. Kushiriki katika mazoezi ya kimwili na kiubunifu ili kuimarisha akili na miili yao.
4. Kuangalia mambo kwa uangalifu, kufikiria kwa kina na kushirikiana na watu wengine katika kutatua matatizo, kujilinda dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na unyonyaji.

2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI

Muhutasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za Awali na Jaduweli la Muhutasari.

2.1 Kurasa za Awali

Sehemu hii inajumuisha utangulizi wa Muhutasari, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo na Madhumuni ya Elimu ya Msingi Zanzibar, pamoja na umuhimu wa kujifunza somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo. Pia, kuna matokeo ya jumla ya kujifunza somo hili. Vipengele nyengine ni; Maelezo kuhusu mawanda na mtiririko wa mada zilizomo, matokeo ya jumla ya darasa husika na ufafanuzi wa vipengele vya jaduweli la ujifunzaji.

2.2 Jaduweli la Ujifunzaji

Sehemu hii inaonesha utaratibu wa ujifunzaji uliobainishwa katika majaduweli matatu yaliyobeba maudhui ya darasa la I mpaka la III. Kila jaduweli limeanza na orodha ya matokeo ya Jumla ya kujifunza kwa darasa linalohusika. Baada ya matokeo ya jumla linafuata jaduweli la ujifunzaji lenye safu wima sita zenye mada, matokeo mahususi ya kujifunza, mbinu za kujifunzia, nyenzo za kujifunzia, upimaji na vipindi kwa kila mada ndogo. Yafuatayo ni maelezo ya kila kipengele katika jaduweli.

2.2.1 Mada

Mada zimejikita katika mawanda ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada husika.

2.2.2 Matokeo Mahususi ya kujifunza

Kila mada ndogo huonesha matokeo mahususi ya kujifunza. Matokeo hayo yanaelezea maarifa, ujuzi na mwelekeo ambao kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo inayohusika. Matokeo mahususi ndiyo yanayotumiwa kufanyia upimaji, ambayo hudokeza viashiria vinavyojenga umahiri. Kwa kawaida, wakati wa kujifunza mwanafunzi huanza kuonesha viashiria hivyo akiwa darasani. Hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kuyafikia matokeo mahususi yaliyotajwa.

2.2.3 Mbinu za Kujifunzia

Safu wima hii imejumuisha mbinu shirikishi za kutumia katika kujifunzia mada za somo hili. Mbinu hizo ni kama vile; maswali na majibu, bungua bongo, onesho mbinu, igizo dhima na mazoezi ya vitendo. Haya ni mapendekezo ya mbinu ambazo zimethibitika kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika vitendo vya kujifunza. Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyengine shirikishi atakazoziona zinafaa kufundishia kulingana na mazingira yake.

2.2.4 Nyenzo za kujifunzia

Nyenzo za kujifunzia huendana na mbinu za kujifunzia, matokeo mahususi ya kujifunza, mada ndogo na mahitaji ya kila mada ndogo. Hata hivyo, nyenzo zilizoorodheshwa ni mapendekezo tu, mwalimu anashauriwa kuwa mbunifu katika kutengeneza nyenzo zinazotokana na mazingira halisi au malighafi za bei nafuu. Aidha, mwalimu ashirikiane na wanafunzi kubuni na kutengeneza zana za kujifunzia kwa kutumia malighafi zilizomo katika mazingira yao.

2.2.5 Upimaji

Katika safu wima hii, zimependekezwa njia za kupima iwapo mwanafunzi amefikia matokeo mahususi ya kujifunza kwa mada husika. Kila siku, wiki mwezi, muhula, na mwisho wa mwaka wa masomo mwalimu anahimizwa kupima maendeleo ya kila mwanafunzi kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizo za upimaji ni kama vile upimaji binafsi, uchunguzi, mkoba wa kazi, orodha hakiki, maswali na majibu na mazoezi.

Wakati wa kuzitumia njia hizo, ni vyema mwalimu akazingatia mapendekezo ya upimaji yaliyomo katika Muhutasari pamoja na kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi.

2.2.6 Vipindi

Hii ni safu wima inayoonesha idadi ya vipindi kwa kila mada inayofundishwa. Idadi hiyo imefikiwa baada ya kujumlisha vipindi vya somo kwa mwaka wa masomo (siku 210) kwa kila darasa. Jumla hiyo imegawika kwa idadi ya mada ndogo zilizomo katika Muhutasari ili kupata wastani wa vipindi kwa kila mada ndogo. Makadirio haya yanaweza kubadilishwa na mwalimu kulingana na mazingira ya ujifunzaji wa mada inayohusika. Mabadiliko hayo yasizidi idadi ya vipindi anavyotakiwa mwanafunzi kufundishwa kwa mwaka.

Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo lina vipindi vitano (5) kwa wiki kwa darasa la I, II na la III. Kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi, muda wa kipindi kimoja ni dakika arubaini (40) kwa mkondo wa asubuhi, na dakika thalathini na tano (35) kwa mkondo wa mchana. Siku ya Ijumaa kila kipindi kitachukua dakika thalathini (30). Utawala wa skuli unatakiwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura zitakazojitokeza.

2.3 Mawanda na Mtiririko

Mada zimepangwa kulingana na makuzi ya wanafunzi ya kiakili, kiroho, kimwili na kihisia. Pia uwezo wao wa kujifunza, umuhimu wa somo katika shughuli za kiuchumi katika jamii yao na kutegemeana kwa mada. Aidha zimezingatiwa mada za maswala mtambuka, hususan ujasiriamali na stadi za maisha.

Mwalimu anashauriwa kufundisha mada hizi kwa kuzingatia mazingira ya kujifunzia na muktadha utakaofaa. Jaduweli lifuatalo linaonesha mpangilio wa mada zilizopendekezwa katika muhutasari.

	MADA	MPANGILIO WA MADA KWA DARASA		
		DARASA LA I	DARASA LA II	DARASA LA III
1.	SANAA YA UCHORAJI	√	√	
2.	SANAA YA UFUNDI	√	√	√
3.	SANAA YA UPAMBAJI			√
4.	HUDUMA YA KWANZA KATIKA MICHEZO	√	√	√
5.	JIMNASTIKI	√	√	√
6.	MAELEKEZO KATIKA MICHEZO	√	√	

	MADA	MPANGILIO WA MADA KWA DARASA		
		DARASA LA I	DARASA LA II	DARASA LA III
7.	MICHEZO MIDOGO MIDOGO	√	√	√
8.	KUOGELEA	√	√	
9.	SHERIA ZA MICHEZO			√
10	KILIMO			√
11	UOKOZI KATIKA MAJI			√
	JUMLA	**07**	**07**	**08**

DARASA LA I

Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la Kwanza

Katika kujifunza somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo kwa Darasa la Kwanza mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1. Kutumia stadi za uchoraji na uundaji wa vitu anuai kwa kuzingatia mbinu za kisasa.
2. Kufanya mazoezi madogo madogo ya unyumbufu, kuimarisha misuli na kutoa huduma ya kwanza kwa usahihi.
3. Kuunda vitu kwa kutumia vifaa vinavyopatikana katika mazingira yake.
4. Kuogelea kwa matendo tafauti na kwa usahihi.
5. Kucheza michezo midogomidogo ya asili na isiyo ya asili.
6. Kufuata maelekezo, kanuni na sheria za michezo tafauti.

DARAZA LA I

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
1. SANAA YA UCHORAJI 1.1 Usanifu wa Herufi na Nambari	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha vifaa vinavyotumika katika uchoraji. ii. Kuchambua makundi ya herufi na nambari katika uchoraji. iii. Kufuatanisha hatua za uchoraji wa herufi na nambari. iv. Kuandaa maumbo ya Herufi na nambari.	• Ugunduzi • Fikiri Jozisha Shirikisha • Matembezi ukumbini • Majadiliano • Changanya kete • Uchunguzi • Kibao fumbo • Onesho mbinu • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Penseli, mistari, rangi, karatasi, vifutio • Manila, Maboksi, • Vipande vya mbao • Mikasi, gundi • Meza • Video inayoonesha usanifu wa herufi na nambari • Projekta • Televisheni • DVD, kompyuta • Modeli ya stensili • Kinasa sauti	• Uchunguzi • Kazi mradi • Usahihishaji rika • Maswali ya papo kwa papo • Orodha hakiki	16
1.2 Uchoraji wa picha za vitu	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**	• Nyimbo • Bungua bongo	• Penseli, rangi, Vifutio	• Kazi mradi	16

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
vya nyumbani	i. Kuainisha vitu vya nyumbani. ii. Kufuata hatua za uchoraji wa picha za vitu vya nyumbani. iii. Kuchora picha za vitu vya nyumbani.	• Uchunguzi • Uwasilishaji kwa TEHAMA • Majadiliano • Matembezi ukumbini • Mchoro huru • Onesho mbinu • Michezo	• Mistari • Manila, maboksi, karatasi • Video inayoonesha uchoraji wa vitu vya nyumbani • Projekta • DVD • Televisheni • Kompyuta • Vitu mbalimbali vya nyumbani • Kinasa sauti	• Tathmini binafsi • Majadiliano • Usahihishaji rika • Mkoba wa kazi	
2. SANAA YA UFUNDI 2.1 Vitu vya nyumbani (Kikombe, sahani, mwiko, sufuria, jagi,	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuelezea hatua za uundaji wa vitu vya nyumbani.	• Nyimbo • Michezo • Uchunguzi • Matembezi ukumbini • Fikiri Jozisha Shirikisha • Majadiliano	• Karatasi, Maboya, Maboksi, Udongo, Majani • Vijiti • Maji, Gundi, Unga wa ngano • Msasa • Viatu vikongwe	• Kazi mradi • Majadiliano • Maswali ya papo kwa papo • Orodha hakiki	16

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
kiti, ndoo na kata).	ii. Kuunda vitu vya nyumbani. iii. Kuelezea utunzaji wa vitu vya nyumbani.	• Ugunduzi • Onesho mbinu • Ziara ya kimasomo • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Vifuu, Madumu, Chupa • Mipira ya kufungia, Kamba • Nyundo, Misumari • Video inayoonesha utengenezaji wa vitu vya nyumbani • Projekta, DVD, Televisheni, Kompyuta, Kinasa sauti		
2.2 Vitu vya skuli (Ubao, meza, kiti, kifutio, debe la kutilia taka, kabati).	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha vitu vya skuli. ii. Kuelezea hatua za kuunda vitu vya skuli.	• Chemsha bongo • Michezo • Hadithi • Uchunguzi • Kibao fumbo • Onesho mbinu • Fikiri Jozisha Shirikisha	• Udongo, majani, maboksi, karatasi • Njukuti, vijiti • Maji, gundi • Viatu vikongwe • Msasa, vipande vya ubao, Madumu • Projekta, DVD	• Maswali na majibu • Kazi mradi • Orodha hakiki • Usahihishaji rika • Selfie	16

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
	iii. Kuunda vitu vya skuli. iv. Kuelezea utunzaji wa vitu vya skuli.	• Matembezi ukumbini • Majigambo • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Televisheni, Kompyuta • Abakasi • Makozi ya mnazi madungudungu, magomba, magurunzi • Video inayoonesha uundaji wa vitu vya skuli. • Rangi nyeusi. • Kinasa sauti • Kibao cha seli ya nukta nundu		
3. HUDUMA YA KWANZA KATIKA MICHEZO	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuelezea dhana ya huduma ya kwanza katika michezo.	• Uchunguzi • Kisa mafunzo • Kumualika mgeni • Ziara ya kimasomo	• Majarida • Video inayoonesha ajali katika michezo • Projekta • DVD • Televisheni	• Majadiliano • Kipimo cha lil • Mkoba wa kaz • Uchunguzi	10

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
3.1 Ajali katika michezo	ii. Kuelezea dhana ya ajali katika michezo. iii. Kufafanua vyanzo vya ajali katika michezo. iv. Kuelezea njia za kuchukua tahadhari kuepukana na ajali.	• Fikiri Jozisha Shirikisha • Majadiliano • Onesho mbinu • Ramani ya dhana • Matembezi ukumbini • Uwasilishaji kwa TEHAMA • Igizo dhima	• Kompyuta • Kinasa sauti		
3.2 Kisanduku cha huduma ya kwanza katika michezo	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuelezea dhana ya Kisanduku cha huduma ya kwanza. ii. Kuchambua faida ya kisanduku cha huduma ya kwanza.	• Chemsha bongo • Michezo • Hadithi • Uchunguzi • Kibao fumbo • Onesho mbinu • Fikiri Jozisha Shirikisha • Matembezi ukumbini • Majigambo	• Projekta, DVD Televisheni, Kompyuta • Video inayoonesha utengenezaji wa kisanduku cha Huduma ya kwanza • Mipira, boksi, Ndoo • Picha za vifaa maalumu vya huduma ya kwanza	• Maswali na majibu • Kazi mradi • Tathmini binafsi • Duara ndani duara nje • Selfie	16

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
	iii. Kutengeneza kisanduku cha huduma ya kwanza.	• Ramani ya dhana • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Majarida • Kisanduku cha huduma ya kwanza		
4. JIMNASTIKI 4.1 Mazoezi ya viungo (Kutembea, kukimbia mbio fupi, kuruka).	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha mazoezi ya viungo. ii. Kufuatanisha hatua za mazoezi ya viungo. iii. Kufanya mazoezi ya viungo.	• Kisa mafunzo • Kumualika mgeni • Ziara ya kimasomo • Fikiri Jozisha Shirikisha • Majadiliano • Onesho mbinu • Ramani ya dhana • Matembezi ukumbini • Michezo • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Koni • Video inayoonesha mazoezi ya viungo • Projekta • DVD • Televisheni • Kompyuta • Kamba • Viatu vya michezo • Filimbi • Vibendera • Tepu • Saa ya kupima muda • Kinasa sauti	• Maswali ya kwa kwa papo • Orodha hakiki • Usahihishaji rika • Uchunguzi • Majadiliano • Ugunduzi	10
4.2 Jimnastiki nyepesi	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**	• Uchunguzi • Kisa mafunzo	• Mkeka wa mazoezi • Filimbi, Maboksi	• Maswali ya kwa kwa papo	15

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
(Mikao, miruko, michupo).	i. Kufafanua aina za jimnastiki nyepesi. ii. Kuelezea hatua za jimnastiki nyepesi. iii. Kufanya mazoezi ya jimnastiki nyepesi.	• Kumualika mgeni • Ziara ya kimasomo • Fikiri Jozisha Shirikisha • Majadiliano • Onesho mbinu • Hadithi • Ramani ya dhana • Matembezi ukumbini • Michezo • Uwasilishaji kwa TEHAMA	Mipira, Koni, Maringi ya gari • Vibao vya mazoezi • Projekta • DVD • Televisheni • Kompyuta • Video inayoonesha jimnastiki nyepesi • Maringi ya baiskeli • Kinasa sauti	• Orodha hakiki • Usahihishaji rika • Uchunguzi • Majadiliano • Ugunduzi • Kadi mrejesho	
5. MAELEKEZO KATIKA MICHEZO	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**	• Onesho mbinu • Matembezi ukumbini • Mazoezi	• Filimbi • Picha za filimbi • Kinasa sauti	• Maswali na majibu • Majadiliano	10

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
5.1 Filimbi katika michezo	i. Kuelezea dhana ya filimbi katika michezo. ii. Kufafanua matumizi ya filimbi katika michezo. iii. Kutumia filimbi katika michezo.	• Kumualika mgeni • Michezo • Fikiri Jozisha Shirikisha		• Msimamo wa dakika tatu • Duara ndani duara nje • Uchunguzi	
5.2 Lugha za ishara katika Michezo	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha ishara zinazotumika katika michezo. ii. Kufafanua matumizi ya ishara katika michezo.	• Michezo • Ziara ya kimasomo • Onesho mbinu • Majadiliano • Kumualika mgeni • Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Video inayoonesha ishara zinazotumika katika michezo • Projekta • DVD • Televisheni • Kompyuta • Vibendera • Filimbi • Picha zinazoonesha lugha ya ishara katika michezo	• Uchunguzi • Kipimo cha liketi • Orodha hakiki	10

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
	iii. Kutumia lugha za ishara katika michezo.		• Kinasa sauti		
5.3 Kanuni za michezo midogo midogo ya watoto (Mbio za mbatata, mbio za miguu mitatu, saka mke wangu na dama).	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha michezo midogo midogo. ii. Kufafanua kanuni za michezo midogo midogo. iii. Kutumia kanuni za michezo midogo midogo katika kucheza.	• Michezo • Onesho mbinu • Majadiliano • Changanya kete • Majigambo • Ugunduzi • Kumualika Mgeni	• Mbatata • Ndoo • Vijiwe • Mapakacha • Kamba • Filimbi • Utepe • Vijiti • Mashanuo • Mafuta • Viti • Vibao • Mipira • Kinasa sauti • Chaki	• Majadiliano • Maswali ya papo kwa papo • Orodha hakiki • Uchunguzi • Mkoba wa kazi	15

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
6. MICHEZO MIDOGO MIDOGO 6.1 Michezo midogo midogo ya asili (Mdako, dama, kinyuri, kinyuki kipenyapenya, majani ya mdimu).	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha michezo midogo midogo ya asili. ii. Kuelezea faida za michezo midogo midogo ya asili. iii. Kutafautisha mbinu katika kucheza michezo midogo midogo ya asili.	• Michezo • Onesho mbinu • Majadiliano • Kumualika mgeni • Ramani ya dhana • Bungua bongo	• Chati za michezo ya asili • Kokoto • Bao • Chaki • Daftari, kalamu • Kinasa sauti	• Dole gumba juu dole gumba chini • Maswali ya papo kwa papo • Usahihishaji rika	14

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
6.2 Michezo midogomidogo isiyo ya asili. (Zumna, karata, kete, keramu, drafti).	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha michezo midogo midogo isiyo ya asili. ii. Kuelezea faida za michezo midogo midogo isiyo ya asili. iii. Kutafautisha mbinu katika kucheza michezo midogo midogo isiyo ya asili.	• Michezo • Majadiliano • Ziara ya kimasomo • Bungua bongo	• Zumna • Karata • Kete • Keramu • Drafti • Daftari, kalamu • Kinasa sauti	• Maswali ya papo kwa papo • Majadiliano • Kipimo cha liketi • Uchunguzi • Tathmini binafsi	12
7. KUOGELEA 7.1 Dhana ya kuogelea	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha vifaa vinavyotumika katika kuogelea.	• Fikiri Jozisha Shirikisha • Michezo • Matembezi ukumbini • Majadiliano	• Miwani ya kuogelea • Nguo za kuogelea • Viatu vya kuogelea • Projekta • DVD • Televisheni	• Majadiliano • Msimamo wa dakika tatu • Uchunguzi	16

MADA	MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA	MBINU ZA KUJIFUNZIA	NYENZO ZA KUJIFUNZIA	UPIMAJI	VIPINDI
	ii. Kujadili faida za kuogelea. iii. Kufafanua kanuni za kuzingatia wakati wa kuogelea.	• Uwasilishaji kwa TEHAMA	• Kompyuta • Boya la kuogelea • Mipira ya gari • Video inayoonesha vifaa vya kuogelea • Kinasa sauti	• Mkoba wa kazi	
7.2 Matendo ya kuogelea	**Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:** i. Kuainisha hatua za kuogelea. ii. Kufuatanisha hatua za kuogelea. iii. Kufafanua faida za kufuata hatua za kuogelea.	• Michezo • Ziara ya kimasomo • Majadiliano • Onesho mbinu • Kumualika mgeni • Uchunguzi	• Miwani ya kuogelea • Nguo za kuogelea • Viatu vya kuogelea • Video inayoonesha matendo ya kuogelea • Boya • Mipira ya gari • Kinasa sauti	• Kipimo cha liketi • Orodha hakiki • Majadiliano • Usahihishaji rika • Duara ndani duara nje	18

DARASA LA II

Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la Pili

Katika kujifunza somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo kwa Darasa la Pili mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1) Kutumia umahiri wa uchoraji, ufinyanzi na uundaji wa vitu anuai kwa kufuata mbinu za kisasa.
2) Kutumia mbinu za utoaji wa huduma ya kwanza kwa aliyechubuka na kuvilia damu.
3) Kufanya mazoezi madogo madogo, jimnastiki kwa uimarishaji wa stadi za michezo mbalimbali.
4) Kusikiliza na kufuata kwa umakini sheria na kanuni zinazowekwa katika michezo.
